# Mtakatifu wa Sioni

*Clôture mois marial* — *Is. 12* — *M: Ami-Fidèle*

**♩ = 70**







*1. Tazameni: ndiye Mungu wa wokovu wangu,*
*namtumainia wala sina wofu tena,*
*kwa kuwa Bwana ni nguvu yangu na wimbo wangu,*
*amekuwa wokovu wangu.*

*2. Nanyi mtateka maji kwenye chemchemi za wokovu.*
*Mshukuruni Bwana, lilieni jina lake*
*Tazameni kati ya mataifa matendo yake makuu;*
*Wakumbusheni ya kuwa jina lake tukufu sana.*

*3. Mwimbieni Bwana, maana ametenda miujiza,*
*Itangazwe duniani kote.*
*Toeni milio ya furaha na shangwe,*
*maana ametukuzwa ndani yako, Mtakatifu wa Sioni.*